





Anansi na hekima Anansi et la sagesse



 Ghanaian folktales
 Wiehan de Jager
 Mutugi Kamundi
 Kiswahili / French
|| Level 3

This story originates from the African Storybook (africanstorybook.org) and is brought to you by Storybooks Canada in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons

[Attribution 3.0 International license.](https://creativecommons.org/licenses/by/3.0)

<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>



Hapo zamani za kale, watu hawakujua chochote. Hawakujua kupanda mimea, hawakujua kushona nguo, wala hawakujua kuunda zana za chuma. Nyame, mungu aliyekuwa mbinguni, ndiye aliyekuwa mwenye hekima zote za dunia. Alihifadhi hekima hiyo kwenye chungu cha udongo.

...

Il y a longtemps, les gens ne savaient rien. Ils ne savaient pas comment faire une récolte, ou comment tisser, ou comment fabriquer des outils de fer. Le dieu Nyame dans le ciel avait toute la sagesse dans le monde. Il la gardait en sécurité dans un pot en argile.



Chungu kilivunjika vipandevipande pale chini. Hekima zikawa za bure kwa mtu yeyote kujichukulia. Na hivyo ndivyo watu walivyojifunza kulima, kushona nguo, kuunda zana za chuma, na mambo yote mengine ambayo watu wanajua kuyafanya.

...

Le pot cassa en mille morceaux sur le sol. La sagesse fut disponible pour tous à partager. Et c'est ainsi que les gens apprirent à cultiver, tisser, fabriquer des outils de fer, et toutes les autres choses que les gens savent comment faire.



Siku moja, Nyame aliamua kumpa Anansi chungu hicho cha hekima. Kila Anansi alipotazama ndani ya chungu cha udongo, alijifunza jambo jipya. Alifurahi sana!

...


Un jour, Nyame décida qu'il donnerait le pot de sagesse à Anansi. Chaque fois qu'Anansi regardait dans le pot en argile, il apprenait quelque chose de nouveau. C'était tellement excitant !



Punde tu alifika juu ya mti, aliwaza, "Natakiwa kuwa ndiye mwenye hekima zote, lakini hapa mwanangu ndiye mwenye akili kuliko mimi." Anansi alikasirishwa sana kiasi kwamba alikitupa kile chungu chini ya mti.

...


Dans peu de temps il atteignit le sommet de l'arbre. Mais il arrêta et pensa, « Je suis supposé être celui avec toute la sagesse et voici que mon fils fut plus sage que moi ! » Anansi était tellement fâché à propos de ceci qu'il lança le pot en argile en bas de l'arbre.



Anansi mlafi alinong'ona moyoni, "Nitakificha chungu hiki juu ya mti mrefu ili nikifaidi mwenyewe." Akasokota uzi mrefu na kuuzungusha kwenye chungu. Kisha, akajifunga tumboni. Akaanza kupanda kwenye mti. Lakini ilikuwa vigumu kupanda kwenye mti huku chungu kikingonga magotini kila mara.

...

Anansi l'avide pensa, « Je vais garder le pot en sécurité en haut d'un grand arbre. Comme ça je pourrai l'avoir à moi seul ! » Il fila un fil long, l'enroula autour du pot en argile et l'attacha à son estomac. Il commença à grimper l'arbre. Mais c'était difficile de grimper l'arbre avec le pot qui le cognait dans les genoux tout le temps.



Wakati huo wote, mwanawe alikuwa amesimama chini ya ule mti akimtamama baba yake. Akamwambia, "Baba, si ingekuwa rahisi kupanda endapo ungekifungia chungu mgongoni?" Basi Anansi akajaribu kukifungia chungu kilichojaa hekima mgongoni mwake, na kweli ikawa rahisi zaidi.

...

Tout le long, le jeune fils d'Anansi avait été debout en bas de l'arbre en train de regarder. « Ne serait-il pas plus facile d'attacher le pot à ton dos plutôt ? » Anansi essaya d'attacher le pot rempli de sagesse à son dos et ce fut vraiment plus facile.